Dailynews 19/04 Pg 3

# Marriage Act amendment to be tabled soon

*Continued from Page 1*

stakeholders on the specific age for Tanzanian girls to get married, insisting that some of the perpetrators of early marriages were the same stakeholders, who were not ready to see marriage age pegged at 18 years.

The current law allows girls below the age of 18 to get married, something that has for long time escalated violence against children eliciting criticism from members of the public.

However, responding, Dr Ndumbaro said that immediately after the ruling of the Court of Appeal which directed the government to amend the law to allow marriage age to be set at 18 years, his ministry brought recommendations in the august House where parliament directed that all stakeholders be engaged before coming up with the new law.

"The views are ready and we expect to table them in the House in the ongoing sessions," said the minister. However, the National Assembly Speaker said that parliament was waiting for the bill and not stakeholders' views.

In a quick response, Dr Ndumbaro said the bill was ready and that it would soon be brought for tabling in parliament.

Earlier during her main question, the MP wanted to know the government's plan to ban marriages for girls below the age of 18.

Responding, Deputy Minister of Community Development, Gender, Women and Special Groups, Mwanaid Ali Khamis said that the government through the ministry of Justice and Constitution Affairs had already collected views from stakeholders on which age a girl should be allowed to get married.

"A comprehensive analysis of stakeholders' views has already been completed and they will be presented in the ongoing parliamentary session for debate in efforts to protect girls so that they can make their dreams come true," said the deputy minister.

Organisations advocating for girls' rights have been pushing the government to fast-track the amendment of the Marriage Act of 1971 article 13 and 17 to make 18 years as the minimum age for marriage as ordered by the High Court and upheld by the Court of Appeal.

In 2016, Tanzania's High Court ruled that two sections of the 1971 Marriage Act that allow girls to marry at 15 with parental consent and 14 with the permission of a court, were unconstitutional.

The court thus ordered the government to amend the Marriage Act within the next year and ruled that the legal marriage age for girls and boys should be recognised as 18 years.

The ruling was made in response to a petition file by Rebecca Gyumi, founder of Msichana Initiative, a local charity promoting girls' rights.

The group argued that the Marriage Act violated girls' rights to equality, dignity and access to education as granted by the constitution.

In their meeting held recently in Dar es Salaam organisations advocating for the girls' rights asked the government to fast-track amendment of the law.

Speaking on behalf of other organisations, Msichana Initiative Director, Rebecca Gyumi, said four years had gone down the lane without implementing the court order.

Ms Gyumi challenged the constitutionality of sections 13 and 17 of the Law of Marriage Act which require consent of parents or court for girls below 18 years before marriage and at the same time, section 13(1) and (2) of the LMA that allows girls to get married at the age of 15 years and boys to get married only upon attaining the age of 18 years.

She therefore sought the declaration that the said provisions were null and void, and must be expunged from the statute and 18 years should remain the minimum marriage age until the Government amends the law.

HabariLeo 19/04 Pg 3

# Serikali kufanya utafiti mmomonyoko wa maadili

Na Anastazia Anyimike, Dodoma

WIZARA ya Katiba na Sheria inatarajia kuunda timu itakayojumuisha wadau wa serikali na wa Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya utafiti kuhusu mmomonyoko wa maadili.

Pia wizara ina mkakati wa kuimarisha maeneo matatu ya sekta ya sheria ambayo ni usuluhishi, uandishi wa miswada ya sheria na majadiliano ya mikataba.

Waziri wa Katibu na Sheria, Dk Damas Ndumbaro amesema hayo Dodoma jana wakati anafungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Dk Ndumbaro alisema inaundwa kamati kutekeleza maelekezo ya Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson ambaye ameiagiza serikali ifanye utafiti kujua ukubwa wa tatizo la mmomonyoko wa maadili.

Alisema alipokea barua ya Bunge ya kuitaka serikali ifanye utafiti kuhusu suala la mmomonyoko wa maadili na amemwelekeza Katibu Mkuu wa wizara hiyo aunde timu ya kushughulikia suala hilo.

"Sasa hivi kuna malalamiko mengi sana na Mheshimiwa Spika (Dk Tulia Ackson) alitoa mwongozo au maelekezo kwa serikali kwamba serikali ifanye utafiti wa mmomonyoko wa maadili ambao unapelekea ongezeko la makosa dhidi ya maadili."

"Jana (juzi) nimepokea barua hiyo na nimemwelekeza Katibu Mkuu aunde timu itakayoshirikisha wadau wote wa serikali Tume ya Mabadiliko ya Sheria kufanya utafiti huo."

Dk Ndumbaro alisema kuanzia sasa hakuna sheria mpya itakayotungwa au kufanyiwa marekebisho bila kufanyiwa utafiti.

Aidha, alisema pia wizara ina mkakati wa kuimarisha maeneo matatu ya sekta ya sheria ambayo ni usuluhishi, uandishi wa mikataba na majadiliano ya mikataba.

Dk Ndumbaro alisema serikali haina mpango wa kuifuta Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na badala yake itaiimarisha kwa kuifanyia mabadiliko sheria.

Aidha, aliwataka wajumbe wa baraza hilo watumie baraza kwenye mambo ya msingi, yenye tija na yenye maslahi kwa wafanyakazi wote na si kuwa chanzo cha vurugu na kuwa jukwaa la kuleta migongano, fitina na uchochezi.

# Mmomonyoko wa maadili kuundiwa timu kuukabili

Ramadhan Hassan, Mwananchi
rhassan@mwananchi.co.tz

**Dodoma**. Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro amemuagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mary Makondo kuunda timu ya wataalamu kushughulikia suala la mmomonyoko wa maadili.

Hatua hiyo inakuja baada ya mwishoni mwa wiki Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson akiwa bungeni kuiagiza Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria ifanye utafiti ni kwa nini kumekuwa na ongezeko la mmonyoko wa maadili nchini.

Akizungumza jana jijini hapa, wakati akifungua kikao cha baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk Ndumbaro alisema hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu mmomonyoko wa maadili na Spika, Dk Tulia Ackson alitoa maagizo kwa Serikali ifanye utafiti ni kwa nini kumekuwa na ongezeko hilo.

Alisema tayari amepokea barua hiyo jana (juzi), na amemwelekeza Katibu Mkuu aunde timu ya wataalamu ili kulishughulikia jambo hilo.

"Bunge limetuelekeza kufanya utafiti, nimemwelekeza katibu mkuu aunde timu kwa kushirikisha wadau wote wa Serikali ili kulitatua jambo hili.

"Wakati tunaingia katika vyama vingi tukasema hawa mabalozi wa nyumba 10 hawana umuhimu lakini tuangalie kazi alizokuwa nazo alikuwa anamjua kila mtu, ana tabia, sifa zipi, kila mgeni akija anajua mgeni huyu ametoka wapi," alisema Dk Ndumbaro.

Alisema ukitaka kwenda mbele lazima uangalie nyuma, ujifunze kutokana na mafanikio na kushindwa kulikotokea ili uchukue uzoefu, kwani mabalozi walikuwa na umuhimu mkubwa.



Wakati tunaingia katika vyama vingi tukasema hawa mabalozi wa nyumba 10 hawana umuhimu, lakini tuangalie kazi alizokuwa nazo, alikuwa anamjua kila mtu, ana tabia, sifa zipi, kila mgeni akija anajua mgeni huyu ametoka wapi, wana umuhimu mkubwa," **Dk Ndumbaro**

Ndumbaro alisema ndio maana anasisitiza hakuna kutungwa sheria ama kufanyiwa marekebisho bila utafiti kufanywa na tume ya kurekebisha sheria.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk Eliezer Feleshi alisema dhumuni la kikao hicho ni kupokea na kujadili taarifa ya mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2023/2024 ya Ofisi ya Mwananseria Mkuu wa Serikali.

Feleshi aliwataka wafanyakazi wa ofisi hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko.

Suala la mmomonyoko wa maadili pia lilizungumziwa na Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango, Januari 29, 2023 katika ibada ya kumsimika Askofu Philipo Mafuja kuwa Askofu wa Kanisa la Afrika Inland Church Tanzania (AICT), Dayosisi ya Pwani.

Dk Mpango aliwaangukia viongozi wa dini akiwataka kukemea vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika jamii, ikiwemo ubakaji na ulawiti akibainisha kuwa vitendo hivyo ni kama vinaanza kuonekana kuwa vya kawaida.

"Nataka kurejea yale nilioon-

Mwananchi 19/04 Pg 2



# Waziri: Tulifanya kosa kubwa kufuta mabalozi wa nyumba 10

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro amekiri serikali ilifanya kosa kufuta mfumo wa mabalozi wa nyumba 10, akiutaja ni uamuzi uliosababisha mmomonyoko wa maadili unaoshuhudiwa sasa nchini.

Dk. Ndumbaro alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa alipofungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Kosa kubwa tulilolifanya ni kufuta mabalozi wa nyumba 10, tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi, tukaona kuwa hawa ni watu wa CCM (Chama Cha Mapinduzi) na kuachana nao, lakini ukweli ni kwamba wale walikuwa na umuhimu mkubwa sana katika jamii zetu.

"(Mabalozi) walikuwa wanamfahamu kila mtu katika eneo lao na kujua tabia za kila mtu, hata kama mgeni akihamia eneo lingine, tabia zake wanazijua, lakini sasa tulipuuza na kuacha kutumia mabalozi wa nyumba 10, hali ambayo inatugharimu hivi sasa," Dk. Ndumbaro alisema.

Waziri huyo alisema tayari wizara yake imeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Bunge kufanya utafiti ili kubaini sababu zinazochangia kuongezeka kwa matukio ya mmomonyoko wa maadili nchini.

"Hivi sasa kumekuwapo malalamiko mengi katika jamii juu ya ongezeko kubwa na mmomonyoko wa maadili na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson hivi karibuni aliniagiza kufanya utafiti ili kubaini nini shida katika hali hii ya kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili," alifafanua.

Dk. Ndumbaro alisema tayari ameshaunda timu ya kufanya utafiti huo na kuja na mapendekezo ambayo yatasaidia kukabilina na ongezeko la makosa ya maadili nchini.

"Lakini pia hivi sasa hakuna sheria ambayo itatungwa ama kufanyiwa marekebisho kama haijafanyiwa utafiti wa kisheria na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Awali waziri huyo aliwataka viongozi wa baraza hilo kutimiza wajibu wao na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia katiba ya nchi, sheria, taratibu, miongozo, mila na desturi za kitanzania.

"Baraza la Wafanyakazi lisiwe sehemu ya kuhamasisha mambo ambayo hayana maslahi kwa taifa letu, lazima mfanye mambo yenu kwa kutetea maslahi ya watumishi mkizingatia katiba ya nchi, sheria, taratibu, weledi na miongozo mbalimbali," aliagiza Dk. Ndumbaro.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi alisema lengo la kikao hicho ni kujadili utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya mwaka 2023/24.

"Kikao hiki pia kitatumika kuendelea kuhimiza watumishi kufanya tathimini ya utendaji wao wa kazi ambao tumekuwa tukiufanya kila wiki," alisema.

Alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 ofisi yake imefanikiwa kuajiri watumishi 50. Kati yao, 48 ni mawakili wa serikali na wawili wataalamu wa TEHAMA.

# Marriage Act amendment to be tabled soon

**From KATARE MBASHIRU in Dodoma**

THE government is expected to table a bill in the ongoing National Assembly restricting girls under 18 years of age to get married, the House heard here yesterday.

The Minister for Justice and Constitution, Dr Damas Ndumbaro, told the august House yesterday that already the government had collected views from all stakeholders concerning the new law, adding that the bill would be ready for the first reading in the ongoing parliamentary budget session.

He was responding to a supplementary question from Special Seats legislator, Dr Thea Ntara (CCM) who had wanted to halt the process for collection of views from

Continues on Page 3

# Muswada Sheria ya Ndoa kutua bungeni

Na FURAHA OMARY, Dodoma

WIZARA ya Katiba na Sheria, imesema ipo tayari kuwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Ndoa utakaohusisha umri wa mtoto kuoa au kuolewa.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jijini hapa jana na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Agnes Hokololo, aliyeuliza kuna mpango gani wa kubadilisha Sheria ya Mirathi ya Kiserikali ya Mwaka 1925 na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Dk. Ndumbaro alisema baada ya Mahakama ya Rufani kutoa uamuzi serikali ibadili umri wa mtoto kuoa au kuolewa, serikali ilipeleka mapendekezo bungeni.

"Bunge likaagiza serikali ikachukue maoni zaidi kutoka kwa wadau mbalimbali, maelekezo hayo tumeyatekeleza tumeyakamilisha na tupo tayari kuja mbele ya Bunge kuwasilisha maoni hayo na mapendekezo," alieleza.

Hata hivyo, Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson, alimweleza Waziri Ndumbaro wanachopaswa kuwasilisha bungeni ni muswada na siyo maoni na mapendekezo ya wadau.

"Hapa bungeni nyie mnapaswa kuleta muswada namaanisha mpo tayari kuleta muswada, maoni na mapendekezo mnayaleta ofisini siyo hapa. Mnaleta muswada au mnaleta maoni na mapendekezo maana maoni na mapendekezo hamuwezi kuleta hapa ndani."

Hata hivyo, waziri huyo alimweleza Spika wapo tayari kupeleka muswada huo.

Awali, akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, alisema suala la mirathi hushughulikiwa na sheria tofauti tatu ambazo ni Sheria ya Kiislamu, Sheria ya Kimila na kwa wasiotumia sheria hizo ikiwemo sheria ya mirathi ya India ya mwaka 1865 ikiwa ni miongoni mwa sheria zilizorithiwa.

Alisema sheria hizo katika kushughulikia suala la mirathi hutumika sanjari na Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 ambayo ndiyo sheria mahususi katika kushughulikia usimamizi wa mirathi yote nchi.

"Wizara imeshaelekeza Tume ya Kurekebisha Sheria nchini kufanyia utafiti sheria zote zikiwemo za mirathi kuziboresha na kuondoa vifungu ambavyo vinakiuka misingi ya haki na usawa. Kuhusu sheria ya ndoa, serikali imeshaandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo na inatarajia kuyawasilisha katika bunge hili linaloendelea," alieleza.

Wakati huo huo, serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria,

# Tume Hakijinai yabaini shida mpya watoto gerezani

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Kuangalia namna ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai imeelezwa makosa yanayoongoza kwa watoto wanaopelekwa mahabusu yanahusu kujamiiana wao kwa wao, mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Tume hiyo inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, ilielezwa hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea vituo vya polisi, mahakama ya watoto na magereza mkoani Dar es Salaam.

Meneja wa Mahabusu ya Watoto jijini Dar es Salaam, Darius Damas, aliiambia Tume hiyo kwamba, mashtaka yanayowakabili watoto ni mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha, ulawiti na ubakaji, matusi, dawa za kulevya na kukutwa na nyara za serikali.

"Kwa ujumla wanakabiliwa na makosa ya mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha; japokuwa na mengine yapo, katika makosa hayo wanakiri na kukutwa wametenda kweli," alisema Damas.

Mahakama, kilichopo wilayani Temeke, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Watoto Kisutu, Vicky Mwaikambo, aliiambia Tume kwamba kati ya kesi zinazoongoza kupokewa kwenye mahakama hiyo, ni zinazohusu watoto kujamiiana wao kwa wao.

"Katika mashauri 852 yaliyoamuliwa ni 750 kwa kipindi cha mwaka jana, kati ya hayo takribani 700 yalihusu madai na mengine jinai, hadi sasa kwa mwaka huu tumepokea mashauri 238 ambayo kati ya hayo, 208 ni madai na jinai 30 jinai," alisema.

"Makosa mengi ya kujamiiana watoto kwa watoto, kwa sababu hapa hatupokei shauri la watu wazima. Ila changamoto ni walioathiriwa kutokubaliana na uamuzi, kwa sababu makosa wanayofanya ni makubwa kuliko adhabu iliyopo kisheria.

Hakimu huyo alishauri kuwapo gereza maalumu kwa ajili ya watoto waliokutwa na makosa kisheria, hasa kwa watenda kosa wa umri kuanzia miaka 15 hadi 17.

Alisema kosa lingine ni kuishi nchini bila kibali, ambalo linalowakuta watoto wanaosafirishwa kwa njia haramu, wakitokea nchi jirani.

"Malezi duni, single mothers (malezi ya mzazi mmoja) ndio changamoto kubwa inayosababisha haya yote. Makosa ya ubakaji na ulawiti kwa watoto yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na utandawazi, kwa kuona kwenye televisheni," alisema.

Pia, alisema sababu nyingine ni watoto kuangalia vipindi visivyofaa kwenye televisheni, kujiunga na makundi rika yasiyo na maadili, ukosefu wa mahitaji muhimu unaomsukuma kuiba na kujaribu mambo mapya kama ulawiti.

Aidha, alisema watoto wanaofikishwa mahabusu hiyo wanapata nafasi ya kurekebishwa tabia kwa kupewa ushauri na unasihi kutoka kwa maofisa ustawi wa jamii, michezo na burudani, kufundishwa ufundi stadi na kazi za mikono pamoja na elimu ya msingi kwa watu wazima, kwa walio na umri wa zaidi ya miaka 14.

Hata hivyo, alisema kituo hicho kinakabiliwa na uchakavu mkubwa wa miundombinu, uhaba wa vitendea kazi kama gari na bajeti ndogo ikilinganishwa na mahitaji.

"Kwa watoto ambao ni waathiriwa wa vitendo hivyo, wapo maofisa ustawi wa jamii ambao wanawapa ushauri nasaha. Ukomo wa kesi makamama ya watoto ni miezi sita. Kwa mwaka 2022 kesi za jinai zilikuwa 132," alisema Hakimu Mwaikambo.

Jaji Othman Chande, akipokea maoni hayo alisema bado sheria zilizopo nchini ikiwamo ya Mtoto ya Mwaka 2009 na mapitio yake imetokana na Sheria ya Mtoto Kimataifa na utekelezaji wake kuwa katika mazingira ya nchi husika.

Tume hiyo pia ilitembelea gereza la Segerea, Ukonga, Chuo cha Taaluma ya Urekebu cha Jeshi la Magereza Ukonga, Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, vituo vya polisi vya Buguruni, Mabatini, Kawe na Mahakama ya Watoto Temeke.

Tume ilipokuwa Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Mkuu wa Chuo hicho, Lazaro Mambosasa, alisema kinachofanyika sasa ni kukipanua na kuboresha mitaala ili kuendana na dunia ya sasa na wapo kwenye hatua za kuanzisha kituo cha utafiti ili iwe rahisi kufanya maboresho yanayohitajika kwa wakati.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Restuta**

# Marekebisho sheria ya mtoto kubaini umri wa kuolewa yaja

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro amesema wizara yake ipo tayari kupeleka muswada bungeni wa marekebisho ya sheria ya mtoto namba 21 ya mwaka 2009 kwa lengo la kubainisha ni umri upi unafaa kuoa au kuolewa.

Ndumbaro alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalumu, Thea Ntara (CCM) aliyetaka kujua ni lini serikali itapeleka marekebisho ya sheria kuhusu sheria hiyo.

Pia aliuliza kwa nini wizara hiyo isiachane na ukusanyaji wa maoni na mapendekezo ya wadau kwani wengi wao ndio wamekuwa wakiona watoto wangali bado wadogo.

Ndumbaro alisema kwamba bunge lilikuwa limeagiza wizara ikusanye maoni ya wadau na mapendekezo kazi ambayo imekamilika. Hivi sasa ipo tayari kuleta muswada wa marekebisho ya sheria bungeni.

Akijibu swali la msingi la mbunge Thea aliyetaka kujua, serikali ina mpango gani wa kuamua kuwa wasichana wasiolewe chini ya miaka 18.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Ali Khamis alisema Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 inatambua mtu mwenye umri chini ya miaka 18 kuwa ni mtoto hivyo ni kosa la jinai kumhusisha na mahusiano ya kimapenzi pia kumuozesha.

Kwa upande mwingine, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu mtoto wa kike kuingia kwenye ndoa akiwa na miaka 14.

Hivyo, serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeshakusanya maoni kutoka kwa wadau kuhusu upi ni umri sahihi wa kuoa na kuolewa.

Uchambuzi wa maoni hayo umeshakamilika na yatawasilishwa ndani ya bunge ili yajadiliwe na mabadiliko kufanyika kadri bunge litakavyoona inafaa ili kumlinda mtoto wa kike afikie ndoto zake.